

06/11/2023

## DCSD Yaadhimisha Siku ya Umoja wa Mataifa na Chaguo Zake Mbalimbali za Kielimu

Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb (DCSD) iliungana na Muungano wa Umoja wa Mataifa wa Marekani (United Nations Association of the USA) - Kitengo cha Atlanta kusherehekea miaka 78 ya shirika hili katika [Siku ya Umoja wa Mataifa](#) katika Shule ya Indian Creek Elementary mnamo siku ya Jumamosi, tarehe 28 Oktoba.

Siku ya Umoja wa Mataifa inasisitiza umuhimu wa kukuza “heshima, usawa, na haki kwa wahamiaji na wakimbizi.” Siku ya Umoja wa Mataifa ya mwaka wa 2023 ilitumika kama ukumbusho unaofaa wa ahadi ya Umoja wa Mataifa ya kutetea haki na ustawi wa wakimbizi na wahamiaji duniani kote. Msimamizi wa DCSD Dkt. Devon Q. Horton alikuwa mmoja wa wazungumzaji wakuu katika maadhimisho hayo na alieleza jinsi Wilaya imeweza kukuza tamaduni, uvumbuzi na malengo.

“Kutoka Dunwoody hadi Damascus, kutoka Tucker hadi Thailandi, kutoka Stone Mountain hadi Siria, kutoka Chamblee hadi Czechoslovakia, na kutoka Lithonia hadi Liberia—katika eneo lote la Marekani na mahali pengine popote ulimwenguni—watoto wote wanastahili elimu ya ubora wa hali ya juu na inayofaa itakayowasaidia kufikia sio tu mafanikio na utimizo lakini pia elimu inayochangia katika jamii bora, shirikishi na yenye tija ambayo inawaleta pamoja watu wote,” Dkt. Horton alisema.

“Kadiri tunavyoshirikiana na kuwa na umoja zaidi kama watu katika kusudi letu, ndivyo tunavyoweza kuwa na nguvu na umoja zaidi kama watu wanaofanya kazi kwa ajili ya wema.”

[Muungano wa Umoja wa Mataifa wa Marekani \(UNA-USA\)](#) ni vuguvugu la Wamarekani waliojitolea kusaidia Umoja wa Mataifa tangu mwaka wa 1945. Ukiwa na zaidi ya wanachama 20,000 na zaidi ya vitengo 200 kote nchini, wanachama wa UNA-USA huungana ili kujitolea kuleta ushirikiano wa kimataifa na matumaini yao ni kwamba kila mmoja wetu anaweza kuchangua katika kuendeleza dhamira ya Umoja wa Mataifa na kufikia malengo ya maendeleo endelevu.

Kama Dkt. Horton anavyoeleza, DCSD ni nyumbani kwa wanafunzi wanaozungumza zaidi ya lugha 140 na wanaowakilisha zaidi ya nchi 180. Wilaya inajivunia kutoa chaguo mbalimbali za masomo.

“Wanafunzi wetu wanatoka karibu kila pembe ya ulimwengu. Kutokana na hili, Shule za Kaunti ya DeKalb zinaendelea kutoa mipango mbalimbali ya kielimu—ikijumuisha shule mbalimbali za mtaala wa STEM hadi mipango ya International Baccalaureate, Charter na Montessori. Hii inatumika kama njia bora za kukuza kipaji cha kila mtoto,” Dkt. Horton alisema.

Kwa picha na video kutoka kwa tukio hili la kulisimua la Siku ya Umoja wa Mataifa la 2023 katika Shule ya Indian Creek Elementary, angalia:

- Picha: <https://www.flickr.com/photos/dekalbschools/sets/72177720312268845/>
- Video: <https://www.youtube.com/watch?v=8iTjmjiQVUM>